



## Ukweli Kuhusu Chanjo ya COVID-19

**Wasiwasi:** Watu walio na mmenyuko wa mzio mkuu hawapaswi kupewa chanjo ya Pfizer/BioNTech

**Ukweli:** Kuwa na mzio wa kitu kimoja hakumaanishi kuwa unao mzio wa kingine. Watu walio na mmenyuko wa mzio kwa kiungo cha chanjo ya COVID-19 hawapaswi kupokea chanjo hiyo.

**Wasiwasi:** Chanjo hiyo imeingizwa sokoni kwa haraka na haijaribiwa vya kutosha kuhusu usalama

**Ukweli:** Chanjo ya COVID-19 imetathminiwa kwa kina katika majaribio makubwa ya kimatibabu. FDA itaidhinisha matumizi yake tu baada ya kupitia data hii.

**Wasiwasi:** Chanjo ya COVID-19 inaweza kusababisha utasa

**Ukweli:** Hakuna ushahidi unaokubaliana na utasa kama madhara ya kando ya chanjo ya COVID-19.

**Wasiwasi:** Chanjo hiyo inapunguza tu dalili lakini haizui kupata au kusambaza COVID.

**Ukweli:** Majaribio yalionesha ya kwamba chanjo hiyo inazuia maradhi ya COVID-19 lakini hayakubaini ikiwa inazuia maambukizi au kuambukiza. Bado hatujui ikiwa inazuia maambukizi au kuambukiza.

**Wasiwasi:** Chanjo hiyo itakuwa ni ya lazima.

**Ukweli:** Wakati chanjo inaidhinishwa kwa matumizi ya dharura, wahasika wanapaswa kukubali kuipokea. Hakuna mipango ya kuifanya chanjo ya COVID-19 kuwa ya lazima.

**Wasiwasi:** Madhara ya kando ya chanjo hiyo ni mabaya kushinda madhara ya kando ya kupata COVID.

**Ukweli:** Chanjo ya COVID-19 inaweza kusababisha uchungu kwenye eneo linalodungwa sindano, maumivu ya kichwa na maumivu ya misuli. Madhara haya ya kando yanaonekana kuwa makali kushinda ilivyo na chanjo nyingi

**lakini yanakwisha kwa siku moja au mbili. Ingawa COVID-19 inaweza kuwa hafifu, inaweza pia kuwa kali zaidi au hata kusababisha kifo.**

---

**Wasiwasi:** *Chanjo hiyo haiwezi kusaidia mwili wako kujenga nguvu za kingamaradhi kama ilivyo na kupata virusi vyenyewe.*

**Ukweli:** **Mwili hujenga kinga dhidi ya COVID katika njia tofauti na chanjo kuliko kwa njia ya maambukizi. Lakini chanjo hiyo husaidia kujenga kingamaradhi bila kupata ugonjwa huo, ambao unaweza kuwa mbaya zaidi au hata kusababisha kifo.**

---

**Wasiwasi:** *Chanjo za mRNA ni hatari zaidi kuliko chanjo zingine.*

**Ukweli:** **Chanjo za Messenger RNA (mRNA) zinaonekana kusababisha madhara ya kando ya muda mfupi mara nyingi zaidi kuliko chanjo zingine nyingi. Lakini madhara haya ya kando hayaonekani kuwa ya kudumu.**

---

**Wasiwasi:** *Chanjo za mRNA zinaweza kuharibu DNA yako*

**Ukweli:** **Chanjo za Messenger RNA hufanya kazi kwa kuzifunza seli mwilini jinsi ya kutengeneza protini inayochochea mwitikio wa kingamaradhi, kwa mujibu wa CDC. Messenger RNA ikidungwa mwilini mwako haitahitilafiana au kuathiri DNA ya chembechembe zako.**

---

**Wasiwasi:** *Ikiwa nilipata COVID-19 na nikapona, sihitaji kupata chanjo hiyo*

**Ukweli:** **Kutokana na athari mbaya zaidi zinazohusishwa na ugonjwa huu na ukweli kuwa kunao uwezekano wa kuambukizwa upya, watu wanashauriwa kupata chanjo ya COVID-19 hata ikiwa wamewahi kupata ugonjwa huu awali.**

---

**Wasiwasi:** *Nikipata chanjo ya COVID-19, ninaweza kukomesha hatua zingine za kiusalama kama vile kuvaa barakoa na kudumisha umbali wa kimwili*

**Ukweli:** **Ingawa chanjo inaweza kukuinga dhidi ya kuwa mgonjwa, haijulikana iwapo unaweza kubeba virusi hivi na kuwaambukiza wengine baada ya kuchanjwa. Hadi tutakapojifunza zaidi, ni bora kuendelea na hatua za kiusalama kama vile kuvaa barakoa na kudumisha umbali wa kimwili.**

---

**Ufikiaji wa hati:** Kwa watu walio na ulemavu au watu wanaozungumza lugha nyingine isiyo Kiingereza, OHA inaweza kutoa taarifa katika mifumo badala kama vile tafsiri, maandishi makubwa au breli. Wasiliana na Kituo cha Taarifa za Afya kwa 1-971-673-2411, 711 TTY au [COVID19.LanguageAccess@dhsosha.state.or.us](mailto:COVID19.LanguageAccess@dhsosha.state.or.us).